**MWONGOZO**

# JARIBIO LA ROYAL

Kenya Certificate of Secondary Education

## 102/2 — KISWAHILI — Kartasi ya 2

**1. UFAHAMU**

a) (i) Wafanyakazi katika matatu na mabasi ni wanaume na shughulizao wanaziendesha kama wanaume na si vinginevyo.

(ii) vyombo vya usafiri vimeundwa kwa kumjali mwanamme na siyo mwanamke au watu wenye tofauti au upungufu Fulani mwilini.

(iii) Katika safari ndefu magari husimama peupe watu waende haja “wakachimbe dawa’ – hali hii haimjali mwanamke.

(iv) Kupanda magari wakati gari li katika mwendo (hasa kwenye matatu) – mwanamke hawezi kufanya hivyo.

(v) wanawake kudanganywa kuwa gari lina viti vya kulala nalo limejaa tele.

**(za kwanza 3 x1 = 3)**

b) (i) Iwapo mwanamke ndiye mwenye mali hiyo, ni ya jamaa yake au mpenzi wa wafanyakazi katika matatu hiyo.

**(1 x 1 = 1)**

c) (i) wanawake wawe na sauti ya umoja na kusema kwamba hili au hiki kinachofanyika siyo sawa au siyo haki kwa mwanamke.

(ii) wanawake wenyewe wajiunge pamoja, kuelimishana na kuanza kupigania haki zao ili wasiendelee kunyanyasika katika vyombo vya usafiri.

(iii) wanawake wasiendelee kuvumilia kutakiwa kuenda haja peupe ilhali ni vigumu kwao kufanya hivyo.

(iv) wanawake waanzishe vuguvugu litakalosaidia usafiri na uchukuzi nchini kuwa wa heshima, kistaarabu na unaowajali wanawake, wazee na watoto.

**(zozote4 x 1 =4)**

d) Marekani, katika mji wa Atlanta, naAfrika Kusini katika mjiwa Johannesburg, wanawake walisusia kupanda magari ya usafiri wa umma na kutembea kwa miguu kwa masafa marefu.

**(1 x 1= 1)**

e) **Huduma za umma**



© TRES 2021

(i) kuzingatia tofauti za kimsingi kati ya wanaume na wanawake ili kuhakikisha kuwa kila mwanajamii anapata huduma anayohitaji kwa amani na usalama na bila usumbufu kwake au kwa wale wanaomtegemea.

(ii) za kila basi la safari ndefu kuwa na choo ndani yake.

(iii) iwe na hadhi ya namna Fulani inayoamuliwa na abiria na wala siyo wenye basi au matatu kwa vile nauli anayolipa ni kura inayotakiwa kumwezesha kuchagua kilicho bora na siyo kilicho duni.

**(zozote4 x 1 =4)**

f) (i) siku za usoni za taifa **(alama 1/0)**

(ii) wakaende haja msituni **(alama 1/0)**

**2. UFUPISHO**

**a) (i) Viwanda hutoa moshi unaosambaa na kuchafuka hewa.**

**(ii) Uchafu unaotupwa ovyo huhatarisha afya ya binadamu**

**(iii) Maji machafu huchafua maji mitoni,maziwani na baharini**

**(iv) Wanyama wengi huharibu misitu,nyasi na vichaka**

**(v) Barabara zaidi zinapojengwa miti hukatwa zinapopitia**

**(vi) Magari hutoa moshi unaoharibuhewa**

**(vii) Ongezeko la watu huharibu misitu ya asili kwa kujiongezea ardhi ya makaazi**

**(Hoja 7 x 1 =7)**

**(b) (i) Kukomesha ujenzi wa viwanda mijini penye watu wengi**

**(ii) Takataka na maji taka kutupwa bila kudhuru afya ya binadamu**

**(iii)Upangaji wa uzazi usisitizwe kuzuia ongezeko la watu**

**(iv) Raia waelimishwe kuhusu madhara ya uharibifu wa mazingira**

**(v)Wahimizwe kupanda miti mingi**

**(vi) Kujenga matuta ya kuzuia mafuriko na kudhibiti mmomonyoko wa** udongo

**(Hoja 6 x 1 =6)**



© TRES 2021

**<u>Utuzaji</u>**

**Sehemu a – 7**

**Sehemu b - 6**

**<u>Utiririko alalma - 2</u>**

**<u>15</u>**

1. **Adhabu – ondoa alama moja kwa kila ziada ya maneno 10 baada ya kumtuza**
2. **Ondoa alama ½ kwa kila kosa la hijai na sarufi (6h na 6s) baada ya kumtuza**
3. **Anayekosa kuandika matayarisho na jibu kwa haya moja asipewe alama za utiririko**

**<u>3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)</u>**

a) Andika tofauti moja kati ya sauti zifutazo. (alama 2)

**(i) /ny/ ni sauti ya kaakaa gumu ilhali /ng'/ ni sauti ya kaakaa laini**

**(ii) /g/ ni kipasuo/kizuiwa ilhali /gh/ ni kikwamizo/kikwamizwa/kikwaruzo**

**(iii) /s/ ni sauti sighuna ilhali /z/ ni sauti ghuna**

**(iv) /ch/ sauti sighuna ilhali /j/ sauti ghuna**

**<u>(Atuzwe½ au0kwakilasehemu 4× ½ =2</u>)**

b) Andika kielezi chenye miundo ifuatayo. (alama 1)

Kipasuo ghuna cha ufizi, irabu ya chini, kati, irabu ya mbele, juu, nazali ya midomo, irabu ya kati chini na tandazwa.**Daima<u>(alama 1 au 0)</u>**

c) (i) Silabi ni nini? (alama 1)

**Ni tamko moja au pigo moja la tamko au mpigo mmoja wa sauti. <u>(alama 1 au 0)</u>**

(ii) Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

**I – <u>o</u>a**

**K - <u>m</u>ti**

**IK - ah**



© TRES 2021

**KI – <u>Tu</u>ta**

**KKI – <u>kwa</u>ke**

**KKKI – <u>mbwe</u>ha**

**KIK – <u>lab</u>da**

**<u>Za kwanza mbili (muundo½ ,mfano ½ )</u>**

d) Eleza dhima tatu za viambishi tamati mbali na kauli ya kutenda/kiishio. (alama 3)

**Ukanusho – haji**

**Kauliyakutendea – som- e- a**

**Undani/kielezi – darasa-ni / mahali asimama-po**

**Wingi / amrisho – amke-ni, cheze-ni**

**Unominishaji/uzoefu – ushona-ji**

**Kiendelezi – amk-e-ni**

**Wakatiacheza-po**

**<u>(Za kwanza 3×1=03)</u>**

e) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi: **-I-** (alama 2)

**Ngeli ya I-I, I-ZI, U-I kwamfano, ilikatwa**

**Ukanusho – kija–siji**

**<u>(2×1=02)</u>**

f) Andika sentensi hii katika ukubwa. (alama 1)

Kijumba chenyewe kilijengwa karibu na mto.

**Jumba lenyewe lilijengwa karibu na jito.<u>(alama 1/0)</u>**



© TRES 2021

g) Taja nomino mbili kutoka ngeli tofauti zinazowakilishwa na kiambishi ngeli kilichopigiwa mstari. (alama 2)

**I**tatumika katika sherehe yake.

Nomino yoyote kutoka ngeli ya **I**-ZI au U-**I** au **I-I**

**Mfano: mikeka, sahani(za kwanza 2×1=02)**

h) Badilisha sentensi katika kauli iliyomo kwenye mabano.

(i) Marie alipewa zawadi yake. (tendeka) (alama 1)

**Marie alipeka zawadi yake. (atunge sentensi upya kwa kutumia kitenzi alichonyambua(alama 1/0)**

(ii) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kishirikishi kipungufu katika ngeli ya KI-VI. (alama 2)

Kitabu **ki** mezani.**(atungesentensi; alama 2/0)**

i) Yakinisha sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili umoja. (alama 1)

Sitaenda nyumbani kesho.

**Utaenda nyumbani kesho. (alama 1/0)**

j) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania katika ngeli ya U-U kutokana na neno: (alama 2)

Zusha

**Uzushi – maneno yasiyo ya kweli**

- **Hali ya kuzua mambo**

  **(alama 2×1=02)**

k) Eleza maana mbili katika sentensi hii.

(alama 2)

Mama anatupa mtoto.

**Mama anamtelekeza mtoto.**

**Mama anamrusha mtoto.**



© TRES 2021

**Mama ametuzawidi mtoto.**

**(Zozote 2×1=02)**

l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)

S – KN(N+Ś)+KT(Ts+T+E)

**Mwalimu aliyetufundisha alikuwa akitembea kitausi.(alama 2/0)**

m) Akifisha: (alama 4)

Akionekana mwenye hasira mkurugenzi huyo alishangaa jameni kwa nini wakenya wanaharibu mali hivi hii si siasa bali ni wendawazimu.

**Akionekana mwenye hasira,mkurugenzi huyo alishangaa, "Jameni!Kwa nini Wakenya wanaharibu mali hivi?Hii si siasa bali ni wendawazimu."(alama 8× ½ =04)**

n) Tunga sentensi kudhihirisha masharti yasiyowezekana katika hali timilifu. (alama 2)

**Angalikuwa amesoma kwa bidii angalikuwa amepita mtihani. (alama 2/0)**

o) Wanne walituzwa na mwalimu. (Tumia kivumishi cha kuorodhesha). (alama 2)

**Mwanafunzi wane alituzwa na mwalimu.(alama 2/0)**

p) Taja vitenzi vyovyote viwili vyenye asili ya kigeni katika kauli ya kutendea. (alama 2)

**Samehea, aminia, salimia, hutubia(alama 2/0)**

q) Ainisha yambwa katika sentensi hii; (alama 3)

Mwanafunzi alitumiwa barua kwa posta.

Yambwa tendwa- barua, yambwa tendewa- mwanafunzi, ala- posta**(alama 3×1=03)**

r) Unda nomino mbili katika hali ya wingi kutokana na kitenzi hiki. (alama 2)

Sawidi

**Miswada, wasawidi (za kwanza 2×1=02)**

s) Biwi ni kwa taka **funda** ni kwa maji na kikuba ni kwa **maua.** (alama 1)

**(alama 2× ½ =01)**



© TRES 2021

3. ISIMU-JAMII (ALAMA 10)

**(a) Sajili ya kitaaluma/hotuba ya kitaaluma/ mwanasayansi**

1. Msamiati wa kisayansi – saratani, kemikali, virutubisho, nitrojeni
2. Lugha kavu – usiyoonyesha hisia bali ya kuafiki kile kinacholengwa
3. Lugha yenye onyo/tahadhari – kemikali hatari kwa miili yetu.
4. Takriri kwa mfano, kemikali

**(Sajili; alama 1, Mfano; alama 1)**

**(b) Sifa za sajili ambazo zingejitokeza**

1. Lugha shawishii kwa mfano, hili ndilo tatizo la kijiji hiki
2. Lugha ya maelezo/ maelekezo – jinsi kemikali zinahatarish amaisha
3. Lugha sanifu inayoeleweka
4. Kuchanganya ndimi
5. Kuhamisha ndimi
6. Matumizi ya takwimu ili kudhihirisha ukweli wa yanayosemwa kwa mfano, asilimia 50%.
7. Lugha ya adabu / heshima/unyenyekevu
8. Sentensi ndefu ndefu ili kujieleza kikamilifu
9. Lugha rasmi - ni ma zingira rasmi

**1**

**(za kwanza 8×1=08)**



© TRES 2021